

Learning by Ear 2012

'Everyone's Different – Respect for Minorities'

Episode 07

The Pygmies of the Democratic Republic of Congo

Author: John Kanyunyu (DRC)

Editor: Friederike Müller, Yann Durand

Characters

<i>Narrator</i>		–m'mume/m'mke, umri miaka 30,
<i>Marie Louise</i> (Mari Luis)	–	m'mke, miaka 40, Kiswahili
<i>Charlotte Souzane</i> (Scharlott Susann)	–	m'mke, miaka 50, Kiswahili
<i>Kavira Manimba</i> (as written)	–	m'mke, miaka 30, Kiswahili
<i>Mathieu Manga</i> (Mattjö Manga)	–	mvulana, miaka 15, Kiswahili
<i>Kazele Soheranda</i> (Kaselé Sso-e-randa)	–	m'mume, miaka 30,

Matamshi:

Mutubé de Masulukwedé : Mutubé de Massulukuedé

INTRO:

Hujambo na karibu kwenye sehemu yetu nyingine ya kipindi cha **Noa Bongo Jenga Maisha Yako**. Kipindi chetu hiki kinaitwa '**Kila mtu ni tofauti- Kuzingatia maslahi ya Jamii za watu walio wachache.**' Leo tunawatembelea mbilikimo wanaoishi katika eneo la mashariki la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Mbilikimo hao ni wakazi wenyeji wanaoishi kwenye makundi madogomadogo katika msitu mkubwa uliopo katika nchi kadhaa za Afrika ya Kati. Kwa ujumla, mbilikimo walio katika eneo hili la Kongo ni wafupi na ngozi zao ni rangi ya maji ya kunde. Tangu jadi, wao ni wawindaji na husaka chakula chao mwituni. Kwa kuwa miti inaendelea kupungua kwenye maeneo fulani ya misitu, watu hao wanapoteza makazi yao ya asili, na hawawezi tena kuishi kama zamani. Kwa hivyo, wengi wanaishi katika viunga vya miji au kwenye vijiji ambako wanakabiliwa na ubaguzi mara kwa mara.

Mbilikimo huchukuliwa kuwa washamba, hivyo basi si watu wengi wanaojishughulisha na utamaduni wao au hali yao. Lakini kwenye kijiji cha Ngite, katika Mkoa wa Kivu Kaskazini, kundi la mashirika yasiyo ya Kiserekali, limewatayarishia mbilikimo hao kambi. Lengo lao ni kuwasaidia mbilikimo kujumuika vyema na watu wengine.

1. SFX/ATMO: Pygmy girls singing (continues under narration)

2. NARRATOR:

Hapa ni Ngite, kwenye kambi ya mbilikimo ya Kubetsi. Kundi la wasichana linatukaribisha kwa wimbo. Kambi yenyewe iko kilomita mia mbili na hamsini kutoka hapo kijijini na ni makazi ya mbilikimo hamsini na watano kutoka familia kumi na sita. Makanisa ndiyo yanayowasaidia kwa makazi hususan Jumuiya ya Makanisa ya Kipentekoste katika Afrika ya Kati.

Song continues, then fades out.

3. NARRATOR

Kambi ya Kubetsi hapo awali, ilikuwa ni makazi ya mababu zao mbilikimo wanaoishi hapa hivi leo. Mbele yetu kuna shamba kubwa la migomba, shamba la mihogo, shamba la mboga na pia shamba la maharagwe. Mbilikimo waishio kwenye kambi hii pia hulima mazao ya vyakula vyao vya asili, kama vile mayugwa na mamumunye. Imewabidi kuingilia kilimo japo hakilingani na maisha yao ya asili ya uwindaji. Mbilikimo maisha yao yamejikita mweituni.

4. CLIP 1: MARIE-LOUISE (Kiswahili)

“Katika kambi hii tunalima maharagwe, mpunga, soya, karanga na biringanya. Tunakula jasho letu. Mavuno yanapopungua sisi huingia mwituni kusaka chakula. Kila mtu hufanya kazi shambani, wanaume na wanawake pamoja.”

5. NARRATOR:

Vigumu sana watu kuacha kabisa mila na desturi zao. Kwa hivyo, mara kwa mara, mbilikimo hao wa Kubetsi hutwaa nyuta, mishale na mikuki yao wakaingia mwituni kuwinda kama walivyofanya siku za awali katika eneo la Mbuga ya Kitaifa ya Virunga. Lakini mbuga hii ni hifadhi ya wanyama; watu hawaruhusiwi kuingia humo na bila shaka ni marufuku kuwinda mbugani humo! Kwa hivyo, watu wanaovuka mpaka na kuingia mbugani, hukabiliana na walinzi wa wanyama pori ambao mara nyingine huwatishia kuwaua.

KW begins

Mbilikimo hao hawapati vitu vyote vya kimsingi katika kambi hiyo. Mathalani, hawapati chumvi, sabuni na nguo. Kwa hivyo, inawabidi kufanya kazi kwa jamii nyingine ili wapate fedha za kununua mahitaji hayo: wanafanya kazi ya kulima mashamba, au

wanaajiriwa kufanya kazi kwenye vinu vya kukamua mafuta, au kazi ya ukwezi.

Hata hivyo, mbilikimo hao daima wanalalamika kwamba hawalipwi fedha za kutosha. Charlotte Souzane anaeleza. Yeye, mara kwa mara, hufanya kazi kwenye mashamba ya watu wanaoishi karibu wanaojiita Wabantu.

6. O-TON 2: *Charlotte Souzane* (Kiswahili)

“Tunapowafanyia kazi, hawatulipi vizuri. Tunazidi kuumia kwa sababu hiyo. Tunafanya kazi siku mbili mfululizo lakini wanaishia kutupatia nusu mkungu wa ndizi na kiasi kidogo cha unga wa sima ama ugali. Laiti wangetulipa japo dola kumi!”

KW ends

7. NARRATOR:

Kambi hiyo ilijengwa kwa madhumuni ya kuwajumuisha mbilikimo hao kwenye jamii nyingine za kienyeji nchini Kongo, hasa Wanande na Wambumba. Lakini uhusiano mara nyingi si mzuri kati ya jamii ya mbilikimo na jamii nyingine. Katika maeneo mengine mbilikimo hawachukuliwi kama binadamu.

Hapo awali, mbilikimo walipozuru maeneo ya jamii nyingine, wakipewa chakula walikuwa wakitengwa na kupelekewa hicho

chakula katika maeneo tofauti, maeneo machafu na mara nyingine karibu na majalala.

Tabia hii inazidi kupungua hasa kutokana na mafunzo ya wachungaji wa makanisa ambayo jamii zote huhudhuria. Charlotte Souzane anasema:

8. CLIP 4: *Charlotte Souzane* (Kiswahili)

“Sasa hivi wanatupatia vyakula kwenye sahani nzuri. Zamani walikuwa wakitupakulia vyakula kwenye majani tena karibu na mashimo ya taka. Walisema walitupatia chakula katika maeneo hayo kwa kuwa hawakutaka kusumbuliwa na harufu za miili yetu. Lakini kwa kuwa tulikuwa tukishiriki ibada pamoja, tukaanza pia kula pamoja.”

9. NARRATOR:

Katika nyanja nyingine, jamii zote zinashirikiana. Kwa mfano shuleni watoto mbilikimo na watoto wengine husoma na kucheza bila kubaguana.

10. SFX 2b: Football match (continues under narration)

11. NARRATOR

Hawa hapa, wakicheza soka, wanafunzi mbilikimo na watoto wa jamii nyingine wanacheza pamoja. Shule ya msingi ya Mutubé de Masulukwedé ilikuwa imejengewa hasa watoto wa mbilikimo. Sasa hivi shule hiyo inawasajili watoto wa jamii nyingine pia. Shule yenyewe ina wanafunzi zaidi ya mia mbili, na miongoni mwao wanafunzi mbilikimo ni ishirini na sita. Watoto mbilikimo husoma bila malipo lakini watoto wa jamii nyingine hutozwa karo kidogo.

12. SFX: Pupil reciting (continues beneath narration)

Watoto wa mbilikimo wamejumuisha ipasavyo ingawa bado kuna matatizo. Kavira Manimba ni mwalimu wa darasa moja la shule hiyo ya msingi.

12. CLIP 4: Teacher Kavira (Kiswahili)

“Ni watulivu darasani, wala hawasumbui wanafunzi wenzao wasiokuwa mbilikimo. Wakati wa kiangazi wana hiari kwenda kuwinda pamoja na wazazi wao. Baada ya msimu huo wao hurudi shuleni tena na kuendelea na masomo yao kama kawaida. Ni werevu, lakini hii tabia ya kutoweka inawatatiza.”

14. NARRATOR:

Matthieu Manga ambaye ni mwanafunzi mbilikimo anafurahia sana mambo anayojifunza shuleni. Anafurahia sana kambi hiyo iliyopo kijijini.

15. CLIP 10: PYGMY MATTHIEU MANGA (Kiswahili)

“Tunapata masomo mazuri shuleni, na tunafundishwa vizuri.

Tunafurahia sisi mbilikimo tunapoishi katika kijiji kimoja pamoja na

Wabantu, na pia tunapofanya kazi katika mashamba yetu yaliyo

kwenye maeneo mbalimbali kijijini mwetu.”

16. NARRATOR

Hata hivyo, ni muhimu kudhibiti ubaguzi uliopo dhidi ya mbilikimo.

Ingawa mashirika mengi yanahimiza watu kujumuika mara

nyingine kuna visa vya ubaguzi katika jamii- kwa mfano kwenye

suala la mapenzi.

KW begins

Watu ambao si mbilikimo wanaweza kuwachumbia au kuwa na

uhusiano wa kimapenzi na mbilikimo, lakini mbilikimo hutatizika

wanapotaka wao kuchumbia. Mara nyingine msichana mbilikimo

akipata ujauzito kwa mvulana ambaye si mbilikimo, huyo mvulana

na familia yake hawakubali ujauzito huo na kwa hivyo msichana huyo anabaki kushughulikiwa na jamaa zake.

Kisa hiki kinaeleza fika jinsi mbilikimo wanavyodharauliwa. Hivi karibuni, kisa kama hiki kilitokea katika kijiji cha Ngite: Mvulana fulani wa kabila la Wanande alimpa ujauzito msichana mbilikimo, kisha akamtelekeza. Mama yake, Charlotte Souzane, anataeleza mambo yalivyokuwa:

17. O-TON 5: *Charlotte Souzane* (Kiswahili)

“Binti yangu alipata mimba, na mvulana anayehusika amekataa katakata. Ndiye binti yangu wa kwanza. Tunamtaka huyu mvulana amuo lakini tayari ameshatoroka. Hajulikani amekimbilia wapi. Baba yake huyu mvulana anasema yuko tayari kumpeleka kituo cha polisi pindi akipatikana kwa hicho kitendo alichofanya.”

KW ends

18. NARRATOR:

Wavulana mbilikimo waliojumuishwa kwenye jamii ya Wakongo wako tayari kuwaoa wasichana kutoka jamii nyingine. Lakini wasichana wasiokuwa mbilikimo si rahisi kwao kuwakubali hao wavulana mbilikimo. Kwa nini?

Kazele Soheranda ni msimamizi wa shughuli za Shirika la Mpango wa kuwasaidia Mbilikimo. Anajua kinachosababisha ubaguzi huo:

19. CLIP 6: Kazele (French)

“Mwanaume mbilikimo anapotaka kuoja, kumchumbia mwanamke Mbantu, anakataa kwa kuzingatia kipato. Mbilikimo wengi huwa maskini... Tunadhani tukidhibiti huo umaskini huenda mambo yatabadilika na mbilikimo watapata hadhi katika jamii. Kwa hivyo, hakuna mtu atakayezingatia hilo suala la mtu kuwa mbilikimo au la.”

20. Musical interlude (Pygmy song - CLIP 7)

21. NARRATOR:

Ubaguzi uishe. Hiyo ndiyo, kaulimbiu ya mashirika mengi yanayoshughulikia masuala ya mbilikimo. Ubaguzi bado upo. Haya mashirika yasiyokuwa ya kiserekali yanafanya kazi gani? Kazele Soheranda wa Shirika la Mpango wa Kuwasaidia Mbilikimo anatulezea kazi yake.

21. CLIP 8: KAZELE (French)

“Katika mikakati yetu ya kufanya kazi tunazingatia mambo yote yanayohusu, kuwajumuisha, kuwaendeleza na pia hadhi ya Jamii ya watu mbilikimo. Katika shughuli zetu zote, tunawahimiza watu mbilikimo kutangamana na watu wa jamii nyingine. Kwa mfano, kwenye elimu hatutaki kutenga shule maalumu kwa mbilikimo. Tunawahimiza wahudhurie shule za kawaida ili wajumuike na jamii nyingine.

KW begins

Na vivyo hivyo, kwenye huduma za afya: wanakwenda kwenye vituo vya afya sawa na watu wengine, na tunashauriana na vituo hivyo vya afya viwafidie fedha wanazotumia. Pia kwenye shughuli nyingine pia mbilikimo na watu wa jamii nyingine daima huwa wakitangamana.”

KW ends

22. NARRATOR:

Kwa mvulana mbilikimo Matthieu Manga, ambaye ni mwanafunzi wa shule ya msingi ya Mutubé de Masulukwedé, ni muhimu sana kuwa na ushirikiano huu na kuheshimiana kati ya mbilikimo na watu wasio mbilikimo.

23: CLIP 9: Pygmy Matthieu (Kiswahili)

“Tunapaswa kuheshimiana ili tuishi vyema duniani. Nadhani tunapaswa kushirikiana kwa kuishi maisha mema. Ninaamini kwamba tukifanya hivyo tunaweza kumaliza kabisa ubaguzi.”

24. SFX: Pygmy girls singing

OUTRO:

Pendekezo hilo la mvulana mbilikimo Mathieu Manga kwa jamii zote kuhusiana na jinsi ya kumaliza ubaguzi, linahitimisha ziara yetu katika jamii ya Mbilikimo huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Mwanahabari wa taarifa hii alikuwa John Kanyunyu, na kipindi hiki ni sehemu ya makala yetu ya **‘Kila mtu ni tofauti-kuzingatia maslahi ya jamii za walio wachache.’** Ukitaka kufahamu zaidi kuhusu kipindi cha **Noa Bongo Jenga Maisha Yako**, au kusikiliza tena sehemu hii au nyingine za makala haya, tafadhali tazama ukurasa wetu wa tovuti, dw.de/lbe. Hadi kipindi kijacho- Kwaheri.